**Kila mtu ana malaika (04) - Kupimwa ukimwi**

Mwandishi: Romie Singh - Mhariri: Saumu Mwasimba

**Waigizaji:**

Angela;
Annie
Daktari
MaTilly (36)
Annie
Djamila
Jet (29)

## Utangulizi

Karibu katika Jifunze kwa Kusikia na mlango ufuatao katika mfululizo wa sehemu 10 za Mchezo wa Kuigiza ambao unafuatiliza maisha ya vijana wanaokabiliana na mibinyo ya aina mbali mbali katika Ulimwengu wa Virusi vya HIV na Ugonjwa wa UKIMWI. Katika mkasa wa leo: Angela, mwenye umri wa miaka 17, tayari ni mjamzito, ana mimba ya miezi saba ambayo ametiwa na mvulana aliyekutana naye mara moja tu katika Party. Kliniki imemtaka arejee tena apokee matokeo ya uchunguzi aliofanyiwa wa Virusi vya HIV. Shoga yake shuleni, Annie, yuko tayari kufuatana naye, lakini Angela anaamuwa kwenda peke yake. Hata hivyo, baada ya kuachana na daktari anaonekana amechanganyikiwa zaidi kuliko alivowahi kuwa hapo kabla. Atamgeukia nani? Utagundua pale utakaposikiliza Mlango huu wa Nne wa "Malaika wa kila mtu".

## Onyesho la Kwanza: Jikoni

| | |
|---|---|
| SFX | Mlio katika mlango ulio wazi: Muziki unatokea ndani |
| ANGELA: | Habari? Annie! |
| ANNIE: | (muziki unazimwa) Angela! Njoo ndani. Mimi karibu niko tayari. (akikaribia MIC) Hebu nipunguze muziki! |
| SFX | Muziki unazimwa. |
| ANNIE: | Unaonekana umechoka Shoga! Angalia huna haja ya kwenda ikiwa huko tayari kutaka kusikia matokeo ya uchunguzi uliofanyiwa. Hamna mtu anayeweza kukulazimisha. Ni uchaguzi wako. |
| ANGELA: | Kweli. Najuwa. Lakini nimeamuwa nitakwenda. Ni tu nahitaji kwenda peke yangu. |
| ANNIE: | Lakini, Angela, nataka kuja pamoja nawe. |
| ANGELA: | Sio. Sikia. Nimefikiria. Ningeweza kungoja kwa saa nyingi, nami niko sawa. Mimi, mimi nahitaji kufikiri kwa utulivu na ukimya. Ningependa kutenda jambo hili mwenyewe, Annie. |

ANNIE: Sawa, ikiwa una hakika. Hutofanya jambo lolote la kipumbavu. Hutofanya?

ANGELA: Hata. Naahidi. Naogopa tu kumwambia mama yangu.

ANNIE: Lakini huhitaji kumwambia. Uchunguzi wa HIV na matokeo yake ni jambo la siri kabisa. Unajuwa. Huhitaji kumwambia mama yako jambo lolote.

ANGELA: Kweli sina haja? Una hakika?

ANNIE: Kabisa. Nilikuweko kliniki kwa ajili ya mambo mengine - unajuwa - kwa ajili ya vidonge vya kuzuwia uzazi. Sio mama yako, sio shule - hamna mtu anayeweza kukwambia useme.

ANGELA: Ahh! Nimepumua. Ahsante Annie.

ANNIE: Kwa hivyo, unajuwa nini cha kutarajia?

ANGELA: Ndio, ndio na sio. Alinipa fomu ambayo nilitia saini. Ah, na kijarida.

ANNIE: Hayo tu? Lakini unahitaji kupewa ushauri nasaha barabara-unajuwa - kuelezea nini maana ya uchunguzi huo.

ANGELA: Kijarida hicho kinasema kuwa umeambukizwa na virusi vya HIV. Lakini hiyo haina maana utakufa. Ndio maana nahitaji kujuwa matokeo yangu.

ANNIE: Nitakuja kukusaidia ikiwa unataka.

ANGELA: (Busu) Sio, lakini nakushukuru kwa kujitolea. Wewe ni malaika!

ANNIE: Hata . Wewe ndio ulio malaika! Mimi sio, angalia maisha yangu!

ANGELA: Kuna malaika kwa kila Annie. Hata kwako! Nitakuja baadae na kukuelezea vipi mambo yalivyokuwa.

ANNIE: Nitakuweko hapa. Naahidi!

## Onyesho la Pili: Hali katika Hospitali

SFX: Penseli inachora karatasi

ANGELA: (kusoma kwa sauti, lakini pole pole, huku akiandika: Hivi virusi ndani yangu mimi ni vipi?)

DAKTARI: Mwengine, aingie (Mlio) Selebi?

ANGELA: Ndio, ni mimi.

DAKTARI: Angela Selebi?

ANGELA: Naam.

DAKTARI: Haya hapa matokeo yako. Wewe una Virusi, POSITIVE.

ANGELA: Ah? Positive? Jee hiyo nzuri?

DAKTARI: Unafikiri POSITIVE ni nzuri? Si nzuri.

ANGELA: Basi NI NEGATIVE.

DAKTARI: Sio, msichana.

ANGELA: Nimesoma kijarida - kimeelezea kuishi kama vile huna virusi.

DAKTARI: (Anapumua) POSITIVE maana yake una virusi.
ANGELA: Lakini, hiyo ina maana nini?
DAKTARI: Wewe hujasoma kijarida.
ANGELA: Nimekisoma na nina masuali fulani.
DAKTARI: Kwa hivyo nenda nyumbani na ukisome tena. Wewe mwenyewe umejitia katika matatizo haya kwa tabia yako ya kipumbavu. Wewe una virusi vya HIV. Hivyo ndivyo ilivyo (muziki unafifia). Mtu mwengine aingine.
SFX Kiunganisho cha muziki.

**Onyesho la Tatu: Hali ilivyo katika mji, taa za barabarani**

ANGELA: (Mlango unagongwa) Hodi? MaTilly?
MA TILLY: Angela! Unamtafuta Annie - Yeye hayuko hapa. Sifahamu aliko - alizungumzia kama vile atakwenda kuzipiga pasi nguo za shangazi. Samahani! Lazima niende ndani. (Anasisimka) Filamu yangu karibu itaanza. Filamu ninayoipenda. Benny punde hivi amepotelewa na mama yake katika ajali ya gari. Na wanamtafuta dada yake ili wamuarifu. Natumai utamuona Annie. Mwambie aje nyumbani kwa haraka.
SFX Mlango unafungwa Televishen iko katika sauti ya juu
SFX Mlio wa hatua za miguu katika changarawe, Simu ya mkono inalia
ANGELA: (akiwa na simu yake ya mkono) Djamila ni wewe? (PUMZIKO) Hakuna mtu nyumbani kwa shangazi, na Annie haonekani mahala popote. Sitaki kuwa peke yangu. (PUMZIKO) Je itakuwa sawa nikija?(PUMZIKO) Ahsante - Nitakuweko huko baada ya dakika 15.
SFX Kiunganisho cha Muziki.

**Onyesho la Nne: Sebuleni. Radio inalia**

ANNIE: Lakini Jet. Nimesema nitakuweko huko kwa Angie pale atakaporudi kutoka kiliniki. Nitaweza kupiga pasi baadae. Nataka kwenda sasa.
JET: (mwenye hasira) Wacha kuniambia nini unachotaka Annie. Nimechoka kusikia nini unachotaka. Ninakupa pesa. Fanya kile ninachosema, Mungu wangu.
ANNIE: Nasikitika, lakini nilimuahidi.
JET (ametulia kidogo) Uliahidi ungesafisha nyumba na kumaliza kupiga pasi. Na yale mashati pale. Nitakuona nitakaporejea. Na lile ni shati langu lililo bora kabisa. Kwa hivyo, kuwa muangalifu.

SFX: Mlango unafunguka/unafungwa. Gari inalia nje na inaondoka. Annie anaanza kuuvumisha wimbo mzuri. Anapandisha sauti juu huku akicheza dansi.

SFX: Gari inasogea. Inasimama. Mlango unafunguka kwa ghafla.

JET: Annie!

ANNIE (anasimama katikati ya maneno) Jet! Unafanya nini hapa? Mola wangu - Pasi!

JET: Nimerejea kutoka kwenye simu yangu - na nini nimegundua? Nakukamata ukiimba na kuunguza langu, langu - shati langu lililo bora kabisa. Nilikwambia uwe muangalifu. Wewe msichana usiokuwa na maana.

SFX Anampiga mkononi

ANNIE: Ah - Jet! Mkono wangu. Unauma. Kweli unauma. (Kilio cha ghafla - kinafifia)

SFX Muziki unafifia chini ya onyesho lifuatalo.

**Onyesho la tano: chumba cha kulala**

ANGELA: (kwa upole, ananusa) Ahsante kwa kuniruhusu kuja hapa na kulia juu ya mabega yako. Djamila. Sijui nini kilichotokea kwa Annie.

DJAMILA: Sawa. Hapa. Chukuwa karatasi nyingine.

ANGELA: (Ananusa) Ahsante. (Mlio) Una chumba kizuri sana na picha nyingi ukutani. Picha ile - ni ya mama na baba yako?

DJAMILA: Ndio, siku yao ya kuowana. Wamependeza sana, ama sivyo?

ANGELA: Kweli. Sijui kweli nani baba yangu. Mama yangu hajawahi kuolewa.

DJAMILA: Ni jambo gumu hilo. Lakini Angela: Nini ambacho kitatokea sasa? Sasa una mimba na mama yako anakuwachia uishi na mtu ambaye humjuwi kabisa. Siamini kile ninachokisikia.

ANGELA (MLIO: Minong’ono kila mahala) Djamila - Kuna kitu kingine - ni lazima uape kwamba hutomwambia mtu ye yote mwengine- si mtu ye yote - unasikia?

DJAMILA: (Wanang’ogona) Naapa kwa jina la Mtume Mtukufu Mohammed, sala na amani zimfikie.

ANGELA: Wiki iliopita pale nilipogundua kwamba nina mimba, daktari alichukuwa damu kuifanyia uchunguzi. Leo nilirejea kwa ajili ya matokeo. Amesema kwamba nina virusi vya HIV.

DJAMILA: Ah Mola wangu. Angela. Mola wangu. Ah!

ANGELA: Unajuwa nini maana pale wanaposema unaweza kuishi nao? Mimi nimechanganyikiwa.

DJAMILA: Lakini ulikwenda kiliniki. Jee daktari hajakuelezea?

ANGELA: Hajafanya hivyo, hilo ndio tatizo. Jee mimi ni mgonjwa? Sijioni mgonjwa. Jee nitumie dawa au nifanye nini?

DJAMILA: Angela - jee mimi sio mtu barabara wa kuuliza. Sisi katika familia yetu hatuzungumzi kabisa juu ya jambo kama hili, ni mwiko. Pindi wakijuwa kwamba wewe ni mjamzito, huenda wakanifukuza na mimi pia.

SFX: KARATASI

ANGELA: (Akisoma) Sikiliza haya: "Virusi vya HIV ni kama vingine. Lakini ni tafauti na virusi vingine tunavyopata." Hiki ndicho kinavyosema kijarida hiki. Lakini sifahamu - na nini tafauti ilioko baina ya virusi vya HIV na Ugonjwa wa UKIMWI. Jee nitakufa? (Kwa sauti kubwa) Na Ant-ee-ret-ro- lolote - Nini kile? Hiki hapa, kisome.

DJAMILA: Shhhhh. Weka sauti yako chini.

ANGELA: (akinong'ona) Niambie kama unaweza kuifahamu.

SFX: KARATASI

DJAMILA: (akisoma polepole) Madaktari bado wanatafautiana wakati gani ulio bora kabisa kuanza matibabu dhidi ya Virusi vya UKIMWI, matibabu yanayoitwa antiretroviral therapy. Baadhi ya madaktari wanapendelea kuanza matibabu pale tarakimu katika CD4 ni juu ya 350. Wengine wanaanza matibabu pale kipimo kinaposhuka kufikia 250. Wewe na daktari wako mtahitaji kuamuwa jambo hilo kwa pamoja.

ANGELA: (kwa sauti kubwa) Aloo, simama kwa hisani yako. Ye yote alioandika hayo anafikiri madaktari ni watu wazuri wenye kutoa misaada. Lakini daktari katika kliniki ya Matula hatonisaidia mimi - hata kidogo.

DJAMILA: Shhh. Angalia. Kuna nambari ya simu hapa ya kuomba msaada. Huenda itakubidi ujaribu kuwapigia. 08000 0123 22 (inategemea nchi). Kwa hivyo watu wengi wana virusi vya HIV. Lazima kuna mtu huko ambaye ataweza kukusaidia.

## Hitimisho

„Malaika wa Kila Mtu“ ni mchezo wa kuigiza ulioandikwa na Romie Singh. Na hayo ndio kutoka JIFUNZE kwa KUSIKIA kwa hii leo. Kwa hisani yako jiunge nasi kwa mkasa wa tano, pale mjomba wa Djamila anamkaribia sana mpwe wake, na Angela anakabiliana na mustakbali mpya usiokuwa wa uhakika.

Kumbuka, ikiwa unataka kukisikiliza kipindi hicho tena au kuwaelezea marafiki juu ya kipindi hiki, kwa hisani yako angalia tovuti yetu www.dw-world.de/lbe Kwa heri.